## BANGI - “Cannabis”

Bangi ikitumiwa huathiri ubongo na kuvuruga utendaji kazi wa mfumo wa fahamu hivyo kubadilisha tafsiri na uhalisia wa vitu. Kemikali inayoathiri ubongo ni tetrahydrocannabinol (THC). Bangi inaongoza kwa matumizi na hufahamika kama msuba, majani, mche, kijiti, blanti, mboga, sigara kubwa, ndumu, msokoto, ganja, skanka, n.k.



Biskuti zenye bangi

Skanka

## MADHARA YA BANGI

- ✓ Huamsha magonjwa ya afya ya akili
- ✓ Kikohozi sugu, pumu, vidonda vya koo na saratani
- ✓ Husababisha uraibu
- ✓ Hupunguza uwezo wa kufikiri na kukumbuka
- ✓ Kuona, kusikia na kuhisi vitu tofauti na uhalisia
- ✓ Kuchochea uhalifu mf; wizi, utapeli na ukatili
- ✓ Huchochea matumizi ya dawa nyingine za kulevya
- ✓ Kupoteza nguvu kazi ya Taifa
- ✓ Huvuruga mahusiano ya kifamilia
- ✓ hupunguza ufanisi kazini na shuleni
- ✓ Husababisha matatizo ya uzazi
- ✓ Kilimo cha bangi huharibu vyanzo vya maji, viumbe hai na uoto asilia
- ✓ Kukosa mwamko wa maendeleo na kusababisha umaskini

## HEROIN

Ni dawa ya kulevya inayopunguza utendaji kazi wa mfumo wa fahamu na kusababisha kupungua kwa mapigo ya moyo na upumuaji. Heroin ni ya pili kwa matumizi Nchini na hufahamika kama unga, ngada, teli (cocktail), msharafu, kijiwe, mdude na brown sugar.



Kete za heroin na Madaraja ya heroin

## MADHARA YA HEROIN

- Magonjwa ya moyo, ini, mapafu, figo, ngozi na meno
- Maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu
- Husababisha arosto yenye maumivu makali
- Husababisha Uraibu
- Huathiri mfumo wa uzazi- kupunguza nguvu za kiume
- Kuharibu mimba, kuzaa watoto njiti au wenye uraibu wa heroin
- Kupoteza nguvukazi ya Taifa
- Mzunguko wa fedha haramu na mfumuko wa bei
- Kupungua kwa hamu ya kula
- Kushuka kwa kinga ya mwili
- Kukosa choo na kusababisha bawasiri
- Mishipa ya damu husinyaa
- Kuweka watu rehani (bondi)
- Vifo kutokana na kuzidisha kiasi

## MIRUNGI- (Khat) “Catha edulis”

Mirungi ni aina ya dawa za kulevya inayochochea mfumo wa fahamu kufanyakazi kuliko kawaida na kusababisha mapigo ya moyo na upumuaji kuongezeka. Kemikali zinazoathiri ubongo ni cathinone na cathine. Mirungi hufahamika kama gomba, miti, gati, mronge, green tea, veve, miraa, mogoka, kangeta, giza, bomba, kashamba, mbaga na alenle



Mirungi

Mtumiaji Mirungi

## MADHARA YA MIRUNGI

- Huongeza shinikizo la damu na kusababisha kiharusi
- Huathiri mfumo wa uzazi- kupunguza nguvu za kiume, ugumba na utasa
- Ajali kutokana na kukosa usingizi
- Magonjwa ya afya ya akili yanayojitokeza kwa vipindi ‘mwezi mchanga’
- Husababisha vidonda kwenye mfumo wa chakula na saratani
- Kuozesha na kubadilisha rangi ya meno, maumivu ya fizi na harufu mbaya mdomoni
- Husababisha magonjwa ya ini
- Hupunguza hamu ya kula
- Kukosa choo na kusababisha bawasiri
- Husababisha uchovu mkali na sonona
- Husababisha ukatili, fujo, ugomvi na migogoro
- Kushusha uzalishaji na kipato

## COCAINE

Ni dawa ya kulevya inayochochea mfumo wa fahamu kufanyakazi kuliko kawaida na kusababisha mapigo ya moyo na upumuaji kuongezeka. Majina maarufu ni pamoja na pele, diego, white sugar, poda nyeupe na sembe.



Kete za cocaine

## MADHARA YA COCAINE

- Husababisha shinikizo la damu, kiharusi au vifo vya ghafla
- Maambukizi ya homa ya ini, VVU na kifua kikuu
- Husababisha msongo wa mawazo, sononа na kutaka kujiua
- Husababisha uraibu
- Huharibu mimba na kuzaa watoto waliodumaa
- Huathiri mfumo wa uzazi - nguvu za kiume, ugumba na utasa
- Huvuruga mahusiano ya kifamilia,
- Hupunguza ufanisi kazini na shuleni
- Mfumuko wa bei na tofauti ya kipato
- Kukosa hamu ya kula
- Hupunguza nguvu kazi ya Taifa
- Kupoteza uwezo wa kunusa
- Kuoza meno
- Kukosa usingizi na kusababisha ajali
- Kushindwa kutimiza majukumu
- Kukithiri kwa rushwa
- Uhalifu – ugaidi, biashara ya binadamu, utakatishaji fedha
- Gharama katika ukamataji, tiba, elimu, nk
- Hasira, ukatili na vurugu
- Vifo kiasi cha matumizi kikizidi.

## DAWA TIBA ZENYE ASILI YA KULEVYA

Ni dawa zinazotumika kwenye tiba lakini zikitumika bila kufuata maelekezo ya daktari huweza kusababisha uraibu. Mf; Valium, Codeine, Oxycodone, Tramadol, Pethidine, Morphine, Ketamine na Fentanyl.

## KEMIKALI BASHIRIFU

Ni kemikali zinazotumika kutengeneza bidhaa mbalimbali lakini zikichepushwa zinaweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya. mf; Acetic Anhydride, Hydrochloric Acid, Ephedrine na Potasium Permanganate.

### Madhara ya Uchepushwaji wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya na Kemikali bashirifu

Kutengeneza dawa zilizo chini ya kiwango, Kuongeza usugu wa dawa na kupelekea madhara mengine kwa watumiaji. Husababisha upungufu wa dawa kwa wahitaji na kuongeza gharama kwa serikali kufidia upungufu huo.

### Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 - Hukumu

1. Kifungo **kisichopungua miaka 30** kwa kulima bangi au mirungi
2. Kifungo **kisichopungua miaka 30** kwa kufanya biashara, kusafirisha au kukutwa na bangi au mirungi **kuanzia kilo 100** na Kifungo cha **maisha zikizidi kilo 100**
3. Kifungo **kisichopungua miaka 30** kwa kufanya biashara, kusafirisha au kukutwa na heroin, methamphetamine au cocaine **isiyozidi gramu 200.**
   Kifungo cha **Maisha zikizidi gramu 200.**
4. Kifungo cha **miaka mitatu** au **faini** ya kuanzia **shilingi laki tano** na isiyopungua **shilingi milioni moja** au **vyote kwa pamoja** kwa kutumia dawa za kulevya.

### Mraibu wa dawa za kulevya hutibiwa kwenye:-


Vitengo vya afya ya akili, Vituo vinavyotoa tiba saidizi kwa kutumia dawa – MAT Clinics, Nyumba za Upataji Nafuu (Sober houses) na Huduma za unasihi kupitia asasi za kiraia.


**Kimetayarishwa na**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya
S.L.P 80327, 8 Barabara ya Kivukoni, 11486 Dar es Salaam
Baruapepe: cg@dcea.go.tz I Tovuti: www.dcea.go.tz

@dceatanzania @dceatanzania @dceatanzania
DCEATV Simu ya Bure 119


# MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA



# DAWA ZA KULEVYA